# MATAMANIO YA VYANZO MBALIMBALI VYA KUJIKIMU KIMAISHA

MRADI ULIYOFANYWA NA CCCEP | MUHTASARI NAMBA 2 | SEPTEMBA 2024

**FOSTA-AFYA**

FoSTA-Afya inafanya kazi na jamili kuelewa vyema matamanio ya mtu binafsi na ya kijumla katika jamii zinazozalisha viungo katika Mkoa wa Tanga, Tanzania.



## KWA NINI NI MUHIMU KUCHUNGUZA MATAMANIO?

Wakulima wadogo ni wadau wakuu katika mabadiliko ya mifumo ya chakula. Matamanio yao yana mchango mkubwa katika kuendesha shughuli zao za kilimo na uwekezaji. Ni muhimu kuelewa mahitaji na matamanio yao, na kuchunguza matamnio hayo kama kichocheo cha maamuzi yao ya kupata riziki. Kuoanisha sera na mbinu za mabadiliko ya mifumo ya chakula na mitazamo pamoja na vipaumbele vyao ni hatua muhimu kwa mafanikio endelevu.

Matamanio yanaathiri kwa kiasi kikubwa maisha ya wakulima na michakato yao ya kufanya maamuzi. Uchunguzi wa matamanio ni muhimu kwa kukuza uelewa wa vichochezi na vikwazo vinavyoathiri maamuzi na vitendo vya wakulima kutoka enzi za zamani, za sasa, na za siku zijazo. Utafiti kuhusu matamanio ulilelenga kuimarisha uelewa wa mapito ya maisha yanayopendelewa na jamii, hususan wakulima, wanawake, na vijana, na kuelewa jinsi wanavyopanga kuyafanikisha.

MATAMANIO NI NINI?

Matamanio yanaweza kufikiriwa kama mahitaji au shauku. Matamanio ya mtu binafsi na ya jamii yanaundwa na muktadha mbalimbali wa kijamii na kitamaduni. Kwa mfano, matamanio yanaweza kuathiriwa na kile kinachotambulika kama vyanzo mbalimbali vya kujikimu maisha. Matamanio ya mtu kuhusu siku zijazo yanategemea kwa kiasi kikubwa jamii anayoishi na tamaduni zake.

Kwa ujumla, matamanio ya watu huongozwa na kile kinachojulikana kama dirisha la matamanio. Hii inahusu taswira walionao kwa kile wanachoamini kuwa kinaweza kufanikishwa. Hivyo, matamanio pia yanaamuliwa na kile watu wanachokiona kilicho karibu nao na kile wanachoona kinaweza kufikiwa.

Wakati huo huo, matamanio yanaweza pia kuathiriwa sana na mazingira yanayowazunguka. Kwa mfano, miradi ya kimaendeleo inayotekelezwa na watendaji kutoka nje ya eneo husika inaweza kuwa na ushawishi mkubwa katika mapendeleo ya wakulima na chaguzi za vyanzo mbalimbali vya kujikimu kimaisha.

Tunatumia mbinu mbalimbali kuchunguza matamanio haya, tukizingatia mambo kama vile umri, jinsia, upatikanaji wa masoko, pamoja na tofauti za maeneo ya ukanda wa juu na ukanda wa chini.

1 Kwa kutumia mahojiano ya kina ya historia simulizi na wazalishaji wa mzao ya viungo, tunachunguza matamanio yao kuhusu mienendo ya vyanzo mbalimbali vya kujikimu kimaisha kuanzia utotoni hadi sasa.

2 Pia, tunazingatia mipango ya baadaye ya mshiriki na watoto wao au jamaa wengine.

3 Kwa kutumia kalenda za matukio, tunabainisha kumbukumbu muhimu, matukio, na mabadiliko ya matamanio kuhusu vyanzo mbalimbali vya kujikimu kimaisha kwa wazalishaji wa mazao ya viungo.

4 Hadi sasa, tumekusanya mahojiano 34 ya historia simulizi kutoka kwa watu wazima wenye umri wa miaka 30 na zaidi.

5 Pia, tumekusanya historia simulizi 8 kutoka kwa vijana wenye umri wa miaka 18 hadi 30 katika maeneo haya.

6 Mbinu ya picha sauti inatumika kuchunguza matamnio kwa kutumia picha mbalimbali.

## UCHAGUZI WA VYANZO MBALIMBALI VYA KUJIKIMU KIMAISHA VINAHUSIANAJE NA MATAMANIO?

Matokeo ya awali yanaonyesha uhusiano wa karibu kati ya uzalishaji wa viungo na matamanio ya wakulima. Kilimo cha viungo kinachukuliwa kuwa shughuli yenye faida kubwa, ambayo inaweza kuwasaidia wakulima kuondokana na umaskini. Wakulima wengi wanatamani kuendelea na hata kupanua uzalishaji wao wa viungo katika siku zijazo. Zaidi ya hayo, kilimo, hususan kilimo cha viungo, kinaonekana kama uti wa mgongo wa uchumi wao. Wakulima wengi pia wanapenda na kutamani kwamba watoto wao waendelee na uzalishaji wa viungo katika siku zijazo.

Hata hivyo, wakulima pia wanatambua changamoto nyingi zinazohusiana na kupanua mashamba na kutegemea uzalishaji wa viungo. Changamoto hizi ni pamoja na msimu wa uzalishaji (hususan kwa karafuu) na mahitaji makubwa ya nguvu kazi wakati wa msimu wa mavuno. Aidha, mabadiliko ya tabianchi, wadudu waharibifu, na magonjwa yanaathiri mavuno na faida kutoka kwa viungo. Hatimaye, masoko yasiyo imara na mabadiliko ya bei yanapunguza matamanio yao, na hivyo kuathiri maono yao kuhusu kile wanachoweza kufanikisha.

Kwa sababu hiyo, wakulima wengi wanatamani kushiriki pia katika shughuli nyingine za kujipatia kipato kama vile biashara ndogo ndogo au kazi ya udereva wa bodaboda. Shughuli hizi hutumika kama 'mbadala' wanapokutana na changamoto zilizotajwa.

Matamanio ya wazalishaji wa viungo mara nyingi huenda nje ya shughuli za kilimo. Hata hivyo, hii haimaanishi kwamba wanataka kuachana kabisa na kilimo cha viungo. Badala yake, wanatamani kupanua vyanzo vyao vya kipato ili kupata utulivu wa kiuchumi na kuweza kuhimili changamoto zitokanazo na uzalishaji wa viungo. Pia, wazalishaji wa viungo mara nyingi hutamani kusaidia watoto wao au jamaa kupitia elimu ya juu, ili kuwapa fursa ya kupata ajira rasmi katika siku zijazo.

## MATAMANIO YA VIJANA

Ingawa vijana wengi wamehusika katika kilimo tangu wakiwa wadogo kwenye mashamba ya familia, kuna mtazamo miongoni mwao kwamba kilimo ni "kazi ngumu" na hakitoi mapato ya haraka kama, kwa mfano, huduma za udereva wa bodaboda.

Hata hivyo, idadi ya vijana wanaojihusisha na uzalishaji wa viungo na biashara ya kilimo inaongezeka – hususan kama kufanya vibarua kwenye mashamba ya viungo na wasafirishaji wa viungo. Hali hii kwa kiasi fulani imetokana na mipango ya maendeleo inayoshawishi matamanio ya vijana. Hata hivyo, ili kuongeza uzalishaji wa viungo miongoni mwa vijana, changamoto zilizotajwa hapo awali zinapaswa kushughulikiwa. Changamoto maalum inayowakumba vijana katika kilimo ni ukosefu wa upatikanaji wa ardhi, jambo linalopunguza matamanio yao kuhusu maendeleo ya kilimo. Vilevile, vijana wa kike wanaonyesha matamanio makubwa ya kufundishwa kuendesha bodaboda, licha ya shughuli hiyo kuonekana kuwa kiume.

## MAPENDEKEZO

- Fikiria jinsi unavyoweza kuchunguza na kujumuisha matamanio tofauti ya wakulima katika kubuni, kutekeleza, na kufuatilia sera na miradi. Malengo ya miradi yanayoendana na matamanio ya wakulima sio tu yana nafasi kubwa ya kufanikiwa na kuwaendelevu, bali pia yanaweza kusaidia watu binafsi na jamii kufanikisha malengo yao.
- Kwa wazalishaji wa viungo katika Mkoa we Tanga, ni muhimu kuhakikisha kwamba sera na utekelezaji vinaakisi matamanio yao sio tu ya kupanua uzalishaji wa viungo, bali pia ya kutanua vyanzo vyao vya kipato.
- Fikiria jinsi sera na utekelezaji unavyoweza kusaidia watu binafsi na jamii kushinda vikwazo vya kimuundo ili kufanikisha matamanio yao – kwa mfano, kuhusu upatikanaji wa ardhi na kuondoa vikwazo vya kijinsia vinavyohusiana na usafiri.









Prepared and disseminated through collaboration with the ESRC Climate Change Centre for Economics and Policy Legacy project led by UoLeeds and Tanzania Forest Conservation Group

To find out more about the project, please visit fosta-health.eu